

KUMSIKILIZA NA KUONGEA NA MTOTO WAKO

NEWCOMER
PARENT
RESOURCE
SERIES



Kuja nchi mpya huathiri familia yako nzima. Kuchukua muda kuunganika, kusikiliza na kuongea na mtoto wako kutamsaidia kuhisi salama zaidi, na inafurahisha sana! Utaweza kumwelea mtoto wako vizuri zaidi unapoweza kuona ulimwengu kupitia macho yake. Utaweza pia kumsaidia nyakati ngumu na kucheka pamoja wakati wa nyakati za kuchekesha. Unapochukua muda wa kusikiliza na kuongea na mtoto wako, humsaidia kuhisi ni wa maana na anapendwa.

Kumsikiliza Mtoto Wako

Kusikiliza uhusisha zaidi ya masikio yako pekee. Mara kwa mara, humanisha kumzingatia mtoto wako kwa makini ili uweze kujua mapema ikiwa ana njaa, amechoka, anaogopa, ana wasiwasi au anataka kusikilizwa. Unapoitikia kwa haraka mahitaji ya mtoto wako, huleta imani. Watoto uhisi vizuri wakati watu wazima muhimu katika maisha yao wanagundua na kujali kuhusu hisia zao. Pia inaweza kuwa njia nzuri ya kutambua na kutaja hisia zao. Kwa mfano, ikiwa mtoto wako analia unapomchukua, unaweza kusema: “Ulimkosa sana Mama. Nilikukosa pia.”

Pia watoto wanataka kukusikiliza wakati unapowasiliza. Jaribu kujua ni nini mtoto wako anachokipenda na ujiunge katika furaha ya kumsaidia kuunda uhusiano thabiti.

Kumsaidia Mtoto Wako Kuongea

WATOTO

Watoto hutazama uso wako na kusikiliza sauti yako. Unapomwangalia na kuongea na mtoto wako, mtoto wako uhisi karibu na wewe. Wakati mtoto wako anapotabasamu au kutoa sauti, huu ni mwazo wake wa kuanza kujifunza kuongea. Watoto wakubwa huwa wanatoka sauti sawa kama yako. Unaweza pia kurudia sauti wanazotoa ili kuwahimiza kuwasiliana.

Mara ya kwanza, mtoto wako hulia ili kukufahamisha anahitaji kitu. Unapompa anachohitaji, anahisi kuwa unamjali. Wakati mwingine ni vigumu kujua ni nini watoto wanataka, lakini sauti yako ya kutuliza na mikono tulivu itamhakikishia mtoto wako unapokuwa ukijaribu kujua (k.m., “Umeumia?” au “Niko hapa.”)

Kati ya umri wa miezi tisa na miezi kumi na minne, kwa kawaida watoto huanza kutumia maneno kivyake, lakini maana ni kubwa zaidi ya neno. (k.m., “Mama” inaweza kumaanisha “Mama ako wapi?” “Nichukue.” au “Huyo ni mama?”)

WATOTO WACHANGA

Watoto wakubwa na wachanga (kati ya umri wa miezi 18 na miaka 2) huelewa polepole lugha zaidi na zaidi. Wanaanza kutumia sentensi za maneno mawili (k.m., “Gari langu.” “Hiyo ni ‘nini?’”) Unapoongea kwa lugha yako ya nyumbani, mtoto wako atakuelewa vizuri zaidi.

Watoto wachanga hujifunza kupitia kucheza. Kuongea kwa lugha yako ya nyumbani na mtoto wako mchanga mnapokuwa mkicheza pamoja kutamsaidia:

- kuendelea kuvutiwa na mchezo wake;
- kulewa na kujifunza kusema maneno;
- kushiriki zaidi katika mchezo wake; na
- kuhisi karibu na wewe zaidi.

WATOTO WA CHEKECHEA

Watoto wanapoendelea kuongea zaidi, maneno yao yanaanza kueleweka zaidi na yanaanza kuwa na umaana wa ndani. Wanaanza kutumia lugha kupata marafiki. Watu zaidi wanapoendelea kuongea na watoto, ndivyo watoto wanajaribu kuongea. Ukiongea na mtoto wako wakati unamtaka afanye kitu pekee, kuna uwezekano mtoto wako hatakusikiliza.

Watoto wadogo wana hamu sana ya kujua mambo na unaweza kutumia hiyo kuanzisha mazungumzo. Wakati watoto wa chekechea wanajifunza kuuliza “kwa nini?” unaweza kuzungumzia kuhusu mambo ambayo yanawavutia na mjifunze pamoja.

Mapendekezo ya Kuboresha Lugha ya Mtoto Wako

1. Zima TV, redio na simu za mkononi. Kupunguza kelele humsaidia mtoto kusikiliza. Punguza muda wa televisheni kuwa saa moja kwa siku. Ondoa vizuizi wakati unataka kuongea na mtoto wako.
2. Endelea kutumia lugha yako ya nyumbani na himiza mtoto wako kujibu kwa lugha yako. (Angalia karatasi ya vidokezo vya Kuendeleza Lugha Yako ya Nyumbani kwa maelezo zaidi.)
3. Msaidie mtoto wako mara hiyo ikiwa anakuhitajika. Hii huonyesha unagundua wakati anahitaji msaada.
4. Inama chini na umpe muda wako wakati mtoto wako anataka kuongea na wewe.
5. Ongea na mtoto wako kuanzia akiwa mtoto mchanga.
6. Tumia maneno rahisi na uliza maswali rahisi.
7. Tengeneza maneno na vifungu vifupi vya mtoto wako kujifunza (k.m., “Zaidi.” “Nisaidie.”).
8. Zungumzia kuhusu unachokifanya na kile ambacho mtoto wako anakifanya.
9. Shiriki vivutio vya mtoto wako mnapokuwa mkicheza pamoja.
10. Ongeza dhana mpya za kucheza ili kumtia moyo mtoto wako kuongea. (k.m., Jifanye kuwa duka kwa kununua na kuuza vitu.)
11. Ongezea kwa yale ambayo mtoto wako anasema.
12. Fanya lugha kuwa ya kucheza kwa kutumia ishara, nyuso, sauti, hadithi michezo au nyimbo tofauti.

Tembelea cmascanada.ca/cnc/parents kwa maelezo zaidi ya lugha mbalimbali ya wazazi



SUPPORTING CHILD CARE IN THE SETTLEMENT COMMUNITY / SOUTIEN DE LA GARDE DES ENFANTS DANS LA COMMUNAUTÉ DE RÈGLEMENT

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada